# Programu kwa Wanafunzi Nje ya Muda wa Shule

## Msaada Nje ya Shule

Katika Ohio, kuna programu ambazo wanafunzi wanaweza kujiunga nazo nje ya muda wa shule. Programu hizi zinaweza kuwa kabla au baada ya shule. Nyingine zinaweza kuwa wakati wa mapumziko ya shule. Programu fulani zinaweza kuandaa msaada wa ziada kwa wanafunzi wanaohitaji msaada na shule. Zinaweza kuwasaidia watoto kufanya vizuri zaidi shuleni kwa kuwapa mahali patulivu pa kufanyia kazi za nyumbani na kufikia kompyuta na intaneti. Zinaweza pia kuandaa msaada wa ziada na kazi za shule au kufanya shughuli za kufurahisha zinazofundisha mambo mapya. Katika programu hizi, watoto wanaweza kupata marafiki wapya na kujifunza kutoka kwa wengine. Huenda familia zikahitaji kumsajili mtoto wao au kufikia sheria fulani. Programu hizi zinaweza kuwa bila malipo au kunaweza kuwa na gharama za ziada. Wengine hata huwapatia watoto chakula au msaada wa usafiri.

## Muhtasari wa Programu

### Programu za Baada au Kabla ya shule

Programu za baada na kabla ya shule mara nyingi hufanyika katika au karibu na shule au ndani ya jamii. Programu hizi huwatia moyo watoto wa umri wote kuboresha stadi zao za kitaaluma, kijamii, na kihisia. Watu waliopata mazoezi huwasaidia wanafunzi na kazi zao za shule na stadi nyingine. Nyakati nyingine, programu hizi huandaa vyakula au milo.

### Kutoa Ushauri

Kutoa ushauri ni wakati mtu anapomsaidia mtu mwingine kujifunza mambo mapya. Hili linaweza kufanyika shuleni au katika jamii. Mshauri ni kama mwalimu au mkufunzi. Humsaidia mwanafunzi na vitu kama kazi ya shule au kujifunza stadi mpya. Washauri wanaweza kuwa watu wazima au wanafunzi wengine walio katika darasa moja au wakubwa zaidi. Programu za kutoa ushauri zinaweza kuwasaidia watoto wafanye mazoezi ya ustadi wao wa Kiingereza na kuunganishwa zaidi na jamii yao. Kutoa ushauri hukuza stadi za

[Copyright] © 2024 Kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE), The Ohio State University 

mawasiliano na huandaa msaada wa ziada na kutia moyo kwa watoto ili wahisi vizuri shuleni.

## Ukufunzi

Wakufunzi wanafanana na mshauri, lakini wanazingatia zaidi masomo ya kitaaluma. Wanaweza kuwafundisha wanafunzi mmoja mmoja au katika vikundi. Programu za ukufunzi huwapa wanafunzi msaada na kazi za kufanyia nyumbani na kazi za shule. Programu fulani za ukufunzi zinaweza kusaidia na masomo hususa kama Kiingereza, hesabu, sayansi, na mengine mengi.

Maktaba fulani za umma zina msaada wa kazi za kufanyia nyumbani, ukufunzi, au programu nyingine bila malipo kwa watoto na familia. Zinaweza pia kuwasaidia wanafunzi na masomo ya mtandaoni. Ili kupata maktaba ya umma karibu nawe, tembelea tovuti ya Library Ohio.

## Kambi za Majira ya Kiangazi

Kambi za majira ya kiangazi (au programu za majira ya kiangazi) hufanyika wakati wa likizo ya majira ya kiangazi. Huwasaidia watoto kujifunza kuhusu mada mbalimbali na kuunganishwa na wengine. Kambi za majira ya kiangazi zinaweza kuangazia zaidi shughuli za kitaaluma, kitamaduni, shughuli za nje, au mazoezi ya kimwili. Kambi fulani zinaweza kuwa na washiriki wa kambi wanaokaa usiku kucha au kwenda kwenye bustani ili kuandaa nafasi zaidi kwa shughuli na kujifunza kuhusu ulimwengu wa asili.

## Programu za Maendeleo ya Vijana

Programu za maendeleo ya vijana zinaweza kutokea katika kipindi chote cha mwaka wa shule katika mazingira ya jamii. Programu hizi zinaangazia kuwasaidia watoto kukuza stadi wanazohitaji kulingana na umri wao.

## Programu za Utamaduni

Programu za kitamaduni huwaruhusu wanafunzi kujifunza zaidi kuhusu tamaduni zao wenyewe na nyingine. Programu hizi hulenga kuwasaidia wanafunzi kuhifadhi utamaduni wao, kujifunza lugha, na kuhisi kwamba wameunganishwa na jamii yao.

[Copyright] © 2024 Kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE), The Ohio State University 

## Mafunzo ya kazi

Programu za mafunzo ya kazi kwa kawaida hutolewa kwa wanafunzi walio katika shule ya sekondari. Wanafunzi hupata uzoefu wa kazi na kujifunza kuhusu fursa mbalimbali za kazi. Programu hizi zinaweza kutolewa kupitia shule, biashara, au mashirika mengine ya jamii. Kwa kawaida, lazima wanafunzi watume ombi na kuchaguliwa.

## Programu za Michezo

Kuna timu mbalimbali za michezo kwa wanafunzi. Timu hizi zinaweza kutokana na jamii au katika shule.

## Programu za Kujitolea

Programu za huduma za kujitolea huwapa watoto na vijana fursa ya kuwa na matokeo mazuri katika jamii zao. Wajitoleaji wanaweza kushiriki katika shughuli kama vile kuchangisha fedha, kupanga matukio, kufundisha, kutoa ushauri, au kufanya kazi kwenye miradi mbalimbali ili kufikia malengo ya programu. Programu hizi kwa kawaida hupangwa na mashirika yasiyo ya faida, mashirika ya kijamii, shule, au mashirika ya serikali. Zinatimiza jukumu muhimu katika kukusanya rasilimali na kuboresha ustawi wa watu binafsi na jamii zilizo na uhitaji.

# Unawezaje kupata programu kwa ajili ya mtoto wako?

Sehemu moja ya kuanzia ni kwa kuwauliza marafiki au washiriki wa familia yako, hasa ikiwa wana watoto. Unaweza pia kuwauliza ikiwa wanajua mashirika yoyote ya kijamii yanayoweza kujua kuhusu programu. Programu nyingi hutolewa na mashirika ya kijamii. Viongozi wa jamii na mashirika ambayo hufanya kazi na familia kama mashirika ya huduma za kijamii, maktaba za umma, makanisa, na hata hospitali zinaweza pia kuwa na habari kuhusu programu.

Unaweza pia kujifunza kutoka kwa shule yako kuhusu programu zinazopatikana kwa ajili ya mtoto wako. Ikiwa huna hakika uanzie wapi, unaweza kumwuliza yeyote katika shule ya mtoto wako. Katika shule ya mtoto wako, walimu, Mwasiliani wa familia, wafanyakazi wa kijamii wa shule, au washauri wa shule wanaweza kujua kuhusu programu mbalimbali

zinazopatikana kwa wanafunzi.

Tembelea orodha yetu ya mashirika ili kujifunza zaidi kuhusu programu na mashirika ya kijamii. Unaweza pia kushiriki habari hii na walimu na wafanyakazi wa shule.

### Ni maswali gani ninayoweza kuuliza ili kujifunza zaidi?

- Ninaweza kwenda wapi ili kujua kuhusu programu za nje ya shule kwa ajili ya mtoto wangu?
- Ni aina gani za programu zinazopatikana nje ya shule ili kuyategemeza masomo ya mtoto wangu?
- Ninaweza kumpeleka wapi mtoto wangu ili apate msaada na kazi zake za kufanyia nyumbani na kazi za shule?
- Mtoto wangu anawezaje kupata msaada na kazi za shule? Mtoto wangu anawezaje kupata msaada na {insert subject area}?
- Ni programu gani zinazowasaidia wanafunzi wa lugha nyingi wanaojifunza Kiingereza?
- Ni programu gani zinazoandaa habari zilizotafsiriwa au zina wakalimani kwa ajili ya wazazi na familia?

## Ninapaswa kutafuta nini ili kujua ikiwa programu fulani ni bora kabisa kwa mtoto wangu?

Unaweza kutumia orodha hii ya maswali ili kukusaidia kuchagua programu kwa ajili ya mtoto wako.

- Programu hii hufanyika wapi?
- Je, mnaandaa usafiri? Je, kuna njia nyingine za usafiri?
- Programu inafanyika lini?
- Lengo la programu hii ni nini?
- Programu hii inategemezaje masomo ya watoto?
- Programu hii inawasaidiaje wanafunzi wanaojifunza Kiingereza?
- Je, mtoto wangu anahisi kukaribishwa na salama katika programu? Je, mimi na familia

yangu tunajihisi huru na kukaribishwa kwenye programu?

- Je, ninahitaji kulipia programu hii? Je, kuna machaguo ya bei nafuu au gharama ya chini?
- Je, wafanyikazi wanawajibika na kujali?
- Je, wafanyakazi wamezoezwa kutoa msaada na mwongozo kwa wanafunzi?
- Je, programu iko katika eneo safi na salama?
- Je, shughuli hizo zinafaana na umri?
- Je, kuna nafasi ya kutosha kwa ajili ya kila mmoja kufanya shughuli hizo?
- Je, programu huandaa ufikiaji wa kompyuta au vifaa vingine ambavyo mtoto wangu huenda akahitaji?
- Je, milo au vyakula huandaliwa?
- Watoto wanahitaji kuhudhuria mara nyingi kadiri gani? Nini kitakachotokea ikiwa mtoto wangu atakosa kikao?

Unaweza kutembelea ukurasa wa Colorin Colorado baada ya programu ya shule ili kujifunza zaidi.

## Kumsajili Mtoto Wako kwa Programu

Unaweza kumwuliza mtu kutoka kwa programu jinsi ya kumsajili mtoto wako. Baadhi ya programu zinaweza kukuhitaji kukamilisha fomu au kuandaa maelezo kumhusu mtoto wako au familia yako. Kumbuka, unaweza kuomba mkalimani au kuwa na habari iliyotafsiriwa kwa lugha unayopendelea. Ikiwa programu hiyo inatoka shuleni, wanatakiwa kuandaa habari kwa familia katika lugha wanayopendelea.

### Unapomsajili mtoto wako:

- ✓ Thibitisha ni lini programu itakapofanyika. Sema, "Acha nihakikishe kwamba nina habari sahihi. Ni lini programu hii itakapofanyika?"
- ✓ Angalia ikiwa programu imefungwa kwa sababu ya likizo au mapumziko yoyote ya pekee. Uliza, "Je, programu imefungwa kwa sababu ya likizo au mapumziko yoyote ya pekee?"

- ✓ Wajulishe ikiwa mtoto wako ana mizio yoyote au vizuizi vya pekee vya lishe. Sema, "Mtoto wangu ana mzio wa [sema mzio alio nao]. Mtoto wangu hawezi kula [sema vizuizi vyake vya lishe ni gani]."
- ✓ Uliza kuhusu ni nini unachopaswa kufanya ikiwa mtoto wako atakosa kuwepo. Uliza, "Ninapaswa kufanya nini ikiwa mtoto wangu atakosa kuwepo? Je, kuna mtu ninayepaswa kuwasiliana naye au kumpigia simu?"
- ✓ Angalia ikiwa mtoto wako anahitaji kuleta vifaa au vitu vya pekee. Uliza, "Je, mtoto wangu anahitaji kuleta vitu au vifaa fulani ili kushiriki katika programu?"
- ✓ Hifadhi habari za mawasiliano za programu kama nambari ya simu, tovuti, au barua pepe. Uliza, "Ninaweza kupata wapi habari kuhusu ni nani wa kuwasiliana naye kuhusu programu hii?"

## Vifaa vya Ziada

- Unaweza kujifunza zaidi kutoka kwa Vifaa vya Familia vya NCELA unapochagua Sura ya 3 "Programu na Huduma Nyingine za Elimu kwa Mtoto Wako" au Sura ya 4 "Kutafuta Shughuli za Ziada kwa Mtoto Wako." Inapatikana katika lugha nne (Kiingereza, Kiarabu, Kichina, na Kihispania). https://ncela.ed.gov/educator-support/toolkits/family-toolkit
- Mradi wa Utetezi wa Watoto huandaa habari kuhusu programu za baada ya shule na majira ya kiangazi katika Ohio. https://cap4kids.org/columbus/after-school-camps
- Mradi wa Utetezi wa Watoto huandaa habari na rasilimali kuhusu programu katika Central Ohio kwa watoto na familia. https://cap4kids.org/columbus/minority-and-immigration-services/resources-for-all-immigrants-and-refugees
- Mbali na upatikanaji wa vitabu bila malipo, maktaba nyingi za umma zina msaada wa bila malipo wa kazi za kufanyia nyumbani, ukufunzi, au programu kwa watoto na familia. Zinaweza pia kuwasaidia wanafunzi na masomo ya mtandaoni na kuwasaidia kufikia kompyuta, intaneti, na teknolojia nyingine ambayo wanaweza kuhitaji. Ili kupata maktaba ya umma karibu nawe, tembelea tovuti ya Library Ohio. https://library.ohio.gov/using-the-library/find-an-ohio-library

[Copyright] © 2024 Kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE), The Ohio State University 

*Vifaa hivi vinalenga kuimarisha ustawi wa kitaaluma, wanafunzi na matokeo ya chuo na kazi kwa wanafunzi wa lugha nyingi wa Ohio. Rasilimali ziliundwa kupitia juhudi ya pamoja kati ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (ODEW) na Kituo cha The Ohio State University cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE) pamoja na kikundi kilichojitolea cha watetezi wa familia, viongozi wa jamii, wafanyakazi wa wilaya ya shule, na walimu.*

[Copyright] © 2024 Kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE), The Ohio State University 